Juhudi za Kuboresha Elimu ya Msingi

Je, mbunge wako anawajibika katika mkoa wako?

Juhudi za Kuboresha Elimu ya Msingi

Je, mbunge wako anawajibika katika mkoa wako?

Shukrani

Kazi hii ya kuandaa kijarida hiki imefanywa na Godfrey Boniventura, wa Idara ya Utafiti na Uchambuzi wa Sera (RPA) katika shirika la HakiElimu.

Mrejesho, mapendekezo na ushauri ulitolewa na Elizabeth Missokia, Robert Mihayo, Elisante Kitulo, na Nyanda Shuli. Tunawashukuru wote kwa michango yao na utayari wao wa kufanya kazi nasi na kufanikisha uandaaji wa kazi hii.

© 2013 HakiElimu

HakiElimu
SLP 79401
Dar es salaam
Simu (255 22) 2151852/3
Faksi (255 22) 2152449

ISBN 978-9987-18-039-4

Sehemu yoyote katika kitabu hiki inaweza kutolewa kwa namna nyingine yoyote kwa madhumuni ya kielimu na siyo ya kibiashara, kwa kuzingatia kuwa chanzo kitatajwa na nakala mbili ziwasilishwe HakiElimu

Utangulizi

Matatizo katika ubora wa huduma katika nchi yetu yanagusa sekta zote, zikiwemo za kilimo, afya, madini na miundombinu. Wakati serikali ina wajibu wa kupanga, kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa mipango yote ya maendeleo, wabunge nao wanao wajibu wa kusimamia na kuhakikisha upangaji bora wa mipango na utekelezaji wake ili mipango hiyo iwe na ufanisi na tija. Wakati tunatambua kwamba kazi ya mbunge jimboni si kuangalia elimu pekee, bali maendeleo kwa ujumla wake katika sekta zote, ni muhimu kukumbushana umuhimu wa elimu katika kuchochea maendeleo ya sekta nyingine zote.

Elimu bora ni kiini na chanzo cha maendeleo mazuri. Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema; "kupanga ni kuchagua". Kama Tanzania ikiamua kuchagua kuboresha elimu ili iwe chachu ya mafanikio ya kujikwamua toka katika umaskini tulio nao, inawezekana. Watu wakielimika, watakuwa na uwezo wa kuleta maendeleo ya kimapinduzi katika kilimo, afya, uwekezaji, mazingira na kijamii. Wabunge wana nafasi kubwa sana katika kuleta mapinduzi ya kubadilisha mfumo wa elimu ili kuinua kiwango cha elimu nchini.

Wabunge wana wajibu wa kuisaidia jamii kuboresha hali ya elimu katika majimbo yao na hatimaye mikoa yao. Wanaweza kuboresha hali hii kwa:

1. kubainisha changamoto za hali ya elimu na kuibana serikali kuboresha hali hiyo,
2. kusimamia mgawanyo wa rasilimali za umma na kuhakikisha mgawanyo huo unalenga vipaumbele na mahitaji ya sekta ya elimu,
3. kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya elimu kwa kuhakikisha utekelezaji wa mipango hiyo unaenda sambamba na malengo ya mpango,
4. kushirikiana na madiwani kusimamia utekelezaji wa mipango ya Halmashauri,
5. kuwaunganisha wananchi kubainisha changamoto za elimu na kuwashirikisha katika kutatua changamoto hizo.

Kijarida hiki kinapima uwajibikaji wa wabunge kwa mwaka 2011/2012 katika kuboresha hali ya elimu ya msingi katika mikoa yao kwa kutumia asilimia kuanzia 0-hadi 100 na madaraja waliyopata kati ya daraja A hadi F. Kijarida hiki kinatoa nafasi kwa wananchi kuweza kuona changamoto au mafanikio yaliyoletwa na wabunge wao na hivyo kuweza kutathmini uwajibikaji wao katika sekta ya elimu; hususani elimu ya msingi. Pia kinatoa nafasi kwa wabunge wenyewe kujitathmini na kuona ni kwa kiwango gani wamefanikisha au hawakufanikisha kuboresha hali ya elimu ya msingi katika mikoa yao.

Methodolojia

Upimaji wa uwajibikaji wa wabunge katika kuboresha elimu katika mikoa yao umetumia viashiria saba ambavyo ni:

1. uandikishaji
2. ikama ya walimu
3. uwiano wa darasa kwa wanafunzi
4. uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi
5. uhaba wa madawati
6. ufaulu
7. idadi ya wahitimu wanaojiunga kidato cha kwanza.

Viashiria vingine kama uwepo wa nyumba za walimu havikutumika kwenye uchambuzi huu kwa sababu ya ukosefu wa taarifa, japo ni muhimu kila wilaya kujitathmini na kujenga nyumba za walimu kadri ya mahitaji yao. Hii ni kwa kuwa nyumba za walimu zina mchango mkubwa katika upatikanaji wa walimu.

Takwimu zote zilizotumika katika kijarida hiki zimetoka kitabu cha Takwimu za Elimu Msingi Tanzania (BEST) 2012[1]. Ili kuwa na usawa wa upimaji wa viashiria vyote, kila kiashiria kimepimwa kwa viwango vinavyoashiria ubora kwa kila kiashiria kama inavyooneshwa katika *jedwali namba 1*. Mikoa mipya ya Geita, Katavi, Njombe na Simiyu, haikuhusishwa[2] katika kipimo hiki.

1 Ni kitabu cha takwimu za sekta ya Elimu cha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi.
2 Mikoa hii ilikuwa bado haijawa mikoa na haimo katika kitabu cha BEST 2012

Jedwali namba 1: Viwango vya kupima viashiria kwa alama na madaraja							
	Alama	**5**	**4**	**3**	**2**	**1**	**0**
	Daraja	**A**	**B**	**C**	**D**	**E**	**F**
1	Uandikishaji	96-100	91-95	86-90	81-85	76-80	< 76
2	Ikama ya walimu	0-40	41-45	46-50	51-55	56-60	> 76
3	Uwiano wa vyoo	0-25	26-30	31-35	36-40	41-45	> 76
4	Uwiano wa darasa	0-40	41-45	46-50	51-55	56-60	> 76
5	Uhaba wa madawati	0 - 5	6 - 10	11 - 15	16-20	21-25	> 76
6	Ufaulu	81-100	61-80	41-60	21-40	0-20	< 76
7	Wanaojiunga kidato cha I	81-100	61-80	41-60	21-40	0-20	< 76

Ukokotoaji wa alama

Alama za jumla za mwisho zimekokotolewa kwa kutafuta wastani wa alama za viashiria vyote vya mkoa husika. Wastani huu umepatikana kwa kujumlisha alama zote za kila kiashiria na kugawanya kwa idadi ya viashiria. Wastani wa alama zote zimekokotolewa katika asilimia ili kupata madaraja. Upimaji huu umetumia alama zifuatazo kupanga madaraja;

81-100=A 61-80=B 41-60=C 21-40=D 0-20=F

Picha za wabunge zilizotumika

Kijarida hiki kimetumia picha nne za wabunge kwa kila mkoa badala ya picha za wabunge wote. Hii haimaanishi kuwa hawa wabunge ambao picha zao zimetumika ndio wamewajibika au kutowajibika. Matokeo haya yamepima wabunge wa mkoa mzima kwa sababu uchambuzi huu umetumia takwimu za mkoa.

ARUSHA

62%=B

Mkoa wa Arusha umekuwa na wastani mzuri wa wanafunzi wanaofaulu ambapo mwaka 2011 asilimia 78.5 walifaulu mtihani wa darasa la saba. Mkoa wa Arusha umefanikiwa kuwa na ikama nzuri ya walimu kwa mujibu wa lengo la kitaifa ambapo mwalimu 1 anafundisha watoto 37 tu. Pia idadi kubwa ya wanafunzi hujiunga kidato cha kwanza. Licha ya mafanikio haya, bado kuna uhaba wa madarasa, matundu ya vyoo na madawati.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Arusha wamepata daraja B?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	96.6	5
Ikama ya walimu	1:40	1:37	5
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:45	1
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:59	1
Uhaba wa madawati	0%	20%	2
Ufaulu wa wanafunzi	100%	78.5%	4
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	75%	4
Jumla ya alama			22
Wastani wa alama			3.1
Wastani wa alama kwa asilimia			62.%
DARAJA			B

DAR ES SALAAM

49%=C

Dar es Salaam imekuwa ikijitahidi kwenye ufaulu wa wanafunzi. Mwaka 2011, asilimia 79.8 ya watahiniwa walifaulu. Pia hakuna tatizo la uhaba wa walimu, ambapo hivi sasa ikama ya walimu ni mwalimu 1 wanafunzi 35. Lakini bado kuna changamoto za zaidi ya wanafunzi 65 kutumia darasa moja na pia wanafunzi 70 kutumia tundu moja la choo. Pia kuna uhaba wa madawati ambapo karibu nusu ya wanafunzi hukaa chini.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam wamepata daraja C?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	93	4
Ikama ya walimu	1:40	1:35	5
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:70	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:65	0
Uhaba wa madawati	0%	48%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	79.8%	4
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	66.9%	4
Jumla ya alama			**17**
Wastani wa alama			**2.4**
Wastani wa alama kwa asilimia			**49%**
DARAJA			**C**

DODOMA

38%=D

Mkoa huu una changamoto nyingi za ubora wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Mkoa huu haujafanikiwa kufikia kiwango hata kimoja kati ya viwango saba vilivyotumika katika upimaji wa utendaji na uwajibikaji wa wabunge kwenye elimu ya msingi katika Mkoa wao. Wabunge wa Mkoa huu wanapaswa kuwajibika zaidi.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Dodoma wamepata daraja D?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	93.1%	4
Ikama ya walimu	1:40	1:47	3
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:62	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:72	0
Uhaba wa madawati	0%	46%	0
Ufaulu wa Wanafunzi	100%	49.4%	3
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	45%	3
Jumla ya alama			**13**
Wastani wa alama			**1.9**
Wastani wa alama kwa asilimia			**38%**
DARAJA			**D**

IRINGA

58%=C

Mkoa wa Iringa umekuwa na wastani mzuri wa wanafunzi wanaofaulu ambapo mwaka 2011 asilimia 69.1 walifaulu mtihani wa darasa la saba. Mkoa wa Iringa umefanikiwa pia kuwa na ikama nzuri ya walimu ya 1:42. Hivyo, juhudi zaidi zinahitajika kutatua tatizo la uhaba wa madawati, madarasa, vyoo na pia kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga kidato cha kwanza.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Iringa wamepata daraja C?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	104	5
Ikama ya walimu	1:40	1:42	4
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:42	1
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:53	2
Uhaba wa madawati	0%	45.4%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	69.1%	4
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	69.9%	4
Jumla ya alama			**20**
Wastani wa alama			**2.9**
Wastani wa alama kwa asilimia			**58%**
DARAJA			**C**

KAGERA

42%=C

Ingawa mkoa huu una wabunge ambao asilimia kubwa ni mawaziri kama Mh Magufuli, Kagasheki na Tibaijuka, bado hawajaweza kuusaidia mkoa wao kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Hivi sasa mwalimu 1 anafundisha watoto 48 badala ya 40. Kuna tatizo la uhaba wa matundu ya vyoo ambapo uwiano ni watoto 60 kwa tundu 1 badala ya 25. Mazingira ya darasani si mazuri, ambapo uwiano wa darasa kwa wanafunzi ni 1:75.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Kagera wamepata daraja C?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	100.2	5
Ikama ya walimu	1:40	1:48	3
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:60	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:75	0
Uhaba wa madawati	0%	53%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	71.6%	4
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	57.5%	3
Jumla ya alama			**15**
Wastani wa alama			**2.1**
Wastani wa alama kwa asilimia			**42%**
DARAJA			**C**

KIGOMA



34%=D

Mkoa huu una wabunge maarufu kama Mh Zitto Kabwe na David Kafulila ambao ni wazuri wa kujenga hoja bungeni lakini hawajaweza kuusaidia Mkoa wa Kigoma kujikomboa kielimu kwa kuihoji na kuihimiza Serikali kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika mkoa wao. Zaidi ya nusu ya wanafunzi wanaomaliza darasa la saba hufeli mtihani wa kuhitimu darasa la saba.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Kigoma wamepata daraja D?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali Halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	85.8	3
Ikama ya walimu	1:40	1:50	3
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:70	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:77	0
Uhaba wa madawati	0%	36%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	44.5%	3
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	44.5%	3
Jumla ya alama			**12**
Wastani wa alama			**1.7**
Wastani wa alama kwa asilimia			**34%**
DARAJA			**D**

KILIMANJARO

82%=A

Mkoa wa Kilimanjaro umekuwa unafanya vizuri sana katika mitihani ya kumaliza darasa la saba ambapo mwaka 2011, asilimia 75 ya watahiniwa walifaulu. Hali ya miundombinu ni nzuri na mkoa umevuka viwango karibu vyote vya mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro wamepata daraja A?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	Zaidi ya 95%	88	3
Ikama ya walimu	1:40	1:32	5
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:28	4
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:42	4
Uhaba wa madawati	0%	1%	5
Ufaulu wa wanafunzi	100%	75.7%	4
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	75.7%	4
Jumla ya alama			**29**
Wastani wa alama			**4.1**
Wastani wa alama kwa asilimia			**82%**
DARAJA			**A**

LINDI

49%=C

Mkoa wa Lindi una hali duni sana ya elimu. Mwaka 2011, asilimia 50.6 ya wanafunzi waliofanya mtihani wa darasa la saba walifeli. Ni moja ya mikoa ambayo kila mara imekuwa inafanya vibaya katika mtihani wa darasa la saba. Mkoa huu una changamoto za miundombinu na mazingira ya kujifunzia ambazo zinahitaji juhudi za makusudi za wabunge wake kuweza kuziboresha. Licha ya changamoto hizo mkoa wa Lindi umefanikiwa katika uandikishaji wa wanafunzi.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Lindi wamepata daraja C?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	101	5
Ikama ya walimu	1:40	1:49	3
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:45	1
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:51	2
Uhaba wa madawati	0%	32.2%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	49.4%	3
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	48.4%	3
Jumla ya alama			**17**
Wastani wa alama			**2.4**
Wastani wa alama kwa asilimia			**49%**
DARAJA			**C**

MANYARA

54%=C

Mkoa wa Manyara umekuwa na wastani mzuri wa wanafunzi wanaofaulu ambapo mwaka 2011 asilimia 69.6 walifaulu mtihani wa darasa la saba. Mkoa wa Manyara umefanikiwa kuwa na ikama nzuri ya walimu ya 1:44 na pia kupunguza uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi. Hata hivyo juhudi zaidi zinahitajika kutatua tatizo la uhaba wa madawati na madarasa.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Manyara wamepata daraja C?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	85.5	3
Ikama ya walimu	1:40	1:44	4
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:34	3
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:60	1
Uhaba wa madawati	0%	37%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	69.6%	4
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	68.6%	4
Jumla ya alama			**19**
Wastani wa alama			**2.7**
Wastani wa alama kwa asilimia			**54%**
DARAJA			**C**

MARA

38%=D

Mkoa wa Mara una hali duni sana ya Elimu. Mwaka 2011 asilimia 49.6 walifeli mtihani wa darasa la saba. Ni moja ya mikoa ambayo imekuwa inafanya vibaya katika mtihani wa darasa la saba. Ni asilimia 38.2 tu ya wahitimu ndio waliojiunga na kidato cha kwanza mwaka 2012. Licha ya mkoa huu kuwa na wabunge maarufu, bado una changamoto za miundombinu na mazingira ya kujifunzia ambazo zinahitaji juhudi za makusudi kutatuliwa.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Mara wamepata daraja D?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	106.4	5
Ikama ya walimu	1:40	1:50	3
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:62	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:79	0
Uhaba wa madawati	0%	52.2%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	51.4%	3
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	38.2%	2
Jumla ya alama			**13**
Wastani wa alama			**1.9**
Wastani wa alama kwa asilimia			**38%**
DARAJA			**D**

MOROGORO

46%=C

Licha ya kuwa na ikama nzuri ya walimu, Mkoa huu una tatizo kubwa la uhaba wa madawati na miundombinu. Upungufu wa madawati ni asilimia 43.5. Wanafunzi zaidi ya 70 wanatumia darasa moja. Idadi ya wanafunzi wanaojiunga kidato cha kwanza si nzuri ambapo asilimia 42 tu ya waliofaulu ndio hujiunga kidato cha kwanza.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Morogoro wamepata daraja C?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	100	5
Ikama ya walimu	1:40	1:41	4
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:53	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:71	0
Uhaba wa madawati	0%	43.5%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	61.4%	4
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	42%	3
Jumla ya alama			**16**
Wastani wa alama			**2.3**
Wastani wa alama kwa asilimia			**46%**
DARAJA			**C**

MBEYA

40%=D

Mkoa huu bado una matatizo mengi ya miundombinu ambapo wanafunzi wanarundikana madarasani kwa wanafunzi zaidi ya 70 kutumia darasa 1. Pia zaidi ya asilimia 41 ya watoto hukaa chini. Ufaulu wa wanafunzi bado si mzuri ambapo asilimia 55 tu walifaulu mwaka 2011. Hali hii imesababisha mkoa wa Mbeya kuwa na idadi ndogo ya wanafunzi wanaojiunga kidato cha kwanza.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Mbeya wamepata daraja D?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	106.1	5
Ikama ya walimu	1:40	1:45	4
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:52	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:76	0
Uhaba wa madawati	0%	41.1%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	55%	3
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	38.9%	2
Jumla ya alama			**14**
Wastani wa alama			**2.0**
Wastani wa alama kwa asilimia			**40%**
DARAJA			**D**

MTWARA

42%=C

Mkoa huu haujafikia viwango vingi vya kitaifa. Kuna upungufu mkubwa sana wa madawati na ndio mkoa unaoongoza kwa wanafunzi kukaa chini ambapo uhaba ni asilimia 85. Hali ya miundombinu si nzuri na pia bado kuna upungufu wa walimu. Takribani nusu ya wanafunzi wanaomaliza darasa la saba hufeli mtihani wa kumaliza elimu ya msingi.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Mtwara wamepata C?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	103	5
Ikama ya walimu	1:40	1:46	3
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:57	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:59	1
Uhaba wa madawati	0%	85.1%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	51.2%	3
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	42%	3
Jumla ya alama			**15**
Wastani wa alama			**2.1**
Wastani wa alama kwa asilimia			**42%**
DARAJA			**C**

MWANZA

40%=D

Mkoa huu una uandikishaji mzuri lakini hali ya mazingira ya kujifunzia na kufundishia si nzuri. Mkoa wa Mwanza una uhaba mkubwa wa vyumba vya madarasa, uhaba wa madawati asilimia 64.5, uhaba wa walimu ambapo mwalimu moja anafundisha wanafunzi 52, uhaba wa matundu ya choo ambapo wanafunzi 77 wanatumia tundu moja.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Mwanza wamepata daraja D?

Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	109	5
Ikama ya walimu	1:40	1:52	2
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:77	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:93	0
Uhaba wa madawati	0%	64.5%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	61.1%	4
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	57.1%	3
Jumla ya alama			**14**
Wastani wa alama			**2.0**
Wastani wa alama kwa asilimia			**40%**
DARAJA			**D**

PWANI

58%=C

Mkoa huu una uandikishaji mzuri wa wanafunzi darasa la kwanza, na pia una ikama nzuri ya walimu. Una wabunge ambao ni mawaziri mfano Mh Kawambwa ambaye ni Waziri wa Elimu na Mafunzo. Licha ya mafanikio hayo, mkoa huu bado una matatizo ya miundombinu inayoathiri wanafunzi kujifunza ipasavyo.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Pwani wamepata daraja C?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	111%	5
Ikama ya walimu	1:40	1:40	5
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:44	1
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:53	2
Uhaba wa madawati	0%	38.4%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	61.8%	4
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	58.4%	3
Jumla ya alama			**20**
Wastani wa alama			**2.9**
Wastani wa alama kwa asilimia			**58%**
DARAJA			**C**

RUKWA



34%=D

Licha ya Mkoa huu kuwa na wabunge maarufu na viongozi wa kitaifa kama vile Waziri Mkuu Mh Pinda, wabunge wa mkoa huu hawajaweza kuusaidia mkoa wao kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Hali ya ufundishaji darasani si nzuri ambapo darasa 1 lina wanafunzi 80. Pia kuna uhaba wa walimu, madawati na tatizo la ukosefu wa vyoo. Mkoa huu haujavuka kiwango hata kimoja cha kitaifa. Asilimia 45 tu ya wahitimu ndio hujiunga kidato cha kwanza.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Rukwa wamepata daraja D?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	88%	3
Ikama ya walimu	1:40	1:49	3
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:51	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:80	0
Uhaba wa madawati	0%	48.5%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	52.5%	3
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	45.3%	3
Jumla ya alama			**12**
Wastani wa alama			**1.7**
Wastani wa alama kwa asilimia			**34%**
DARAJA			**D**

RUVUMA

46%=C

Mkoa wa Ruvuma hadi hivi sasa ndio unaongoza kwa kuwa na asilimia 107 ya udahili wa wanafunzi wenye umri wa kwenda shule. Jitihada kubwa zimefanyika kupunguza uhaba wa madawati, ambapo hivi sasa uhaba ni asilimia 24. Hali ya ufaulu si nzuri ambapo zaidi ya nusu ya wanafunzi hufeli mtihani. Pia kuna changamoto ya uhaba wa walimu na madarasa.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Ruvuma wamepata daraja C?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	107.7	5
Ikama ya walimu	1:40	1:48	3
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:50	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:56	1
Uhaba wa madawati	0%	24%	1
Ufaulu wa wanafunzi	100%	46.2%	3
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	46%	3
Jumla ya alama			**16**
Wastani wa alama			**2.3**
Wastani wa alama kwa asilimia			**46%**
DARAJA			**C**

SINGIDA

32%=D

Licha ya kuwa na wabunge mahiri wa kujenga hoja bungeni kama Mh Lissu, Nchemba na Nyarandu ambaye ni waziri, Mkoa wa Singida umekuwa ukifanya vibaya katika matokeo ya mtihani wa darasa la saba. Mkoa huu unakabiliwa na changamoto zinazoathiri ufundishaji na ujifunzaji. Hivi sasa mwalimu 1 anafundisha watoto 70 badala ya 40. Kuna tatizo la uhaba wa matundu ya vyoo ambapo uwiano ni watoto 85 kwa tundu 1 badala ya 25. Mazingira ya darasani pia si mazuri, ambapo uwiano wa darasa kwa wanafunzi ni 1:112.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Singida wamepata daraja D?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	90.4	3
Ikama ya walimu	1:40	1:70	0
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:85	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:112	0
Uhaba wa madawati	0%	18%	2
Ufaulu wa wanafunzi	100%	46.8%	3
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	41%	3
Jumla ya alama			**11**
Wastani wa alama			**1.6**
Wastani wa alama kwa asilimia			**32%**
DARAJA			**D**

SHINYANGA

34%=D

Mkoa wa Shinyanga una hali duni sana ya Elimu. Kwa miaka 6 mfululizo, mkoa huu umekuwa ukishika nafasi ya pili kutoka mwisho kwa kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanaofeli. Mwaka 2011 asilimia 57.7 walifeli mtihani wa darasa la saba. Mkoa huu una tatizo kubwa la miundombinu.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Shinyanga wamepata daraja D?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	88.7	3
Ikama ya walimu	1:40	1:49	3
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:77	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:77	0
Uhaba wa madawati	0%	46%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	57.7%	3
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	46.8%	3
Jumla ya alama			**12**
Wastani wa alama			**1.7**
Wastani wa alama kwa asilimia			**34%**
DARAJA			**D**

TABORA

40%=D

Ingawa mkoa wa Tabora una wabunge maarufu na baadhi yao ni mawaziri na licha ya ukweli kuwa mkoa huu una bahati ya kuwa baadhi ya wabunge wake kama vile Margaret Sitta na Juma Kapuya wamewahi kuwa mawaziri wa elimu, wabunge wa Tabora hawajaweza kutumia nafasi zao kiushawishi kuuletea maendeleo ya elimu ya msingi mkoa huu. Mkoa huu una uhaba mkubwa wa walimu, madarasa, matundu ya vyoo, na madawati. Kiujumla mkoa wa Tabora una mazingira duni ya kufundishia na kujifunzia.

Kwa nini wabunge wa Mkoa wa Tabora wamepata daraja D?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	92.7%	4
Ikama ya walimu	1:40	1:46	3
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:69	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:88	0
Uhaba wa madawati	0%	48.6%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	47.4%	3
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	62.4%	4
Jumla ya alama			**14**
Wastani wa alama			**2**
Wastani wa alama kwa asilimia			**40%**
DARAJA			**D**

TANGA

38%=D

Mkoa huu una changamoto nyingi za ubora wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Mkoa huu haujafanikiwa kufikia viwango sita kati ya viwango saba vilivyotumika katika upimaji wa utendaji na uwajibikaji wa wabunge kwenye Elimu ya Msingi katika Mkoa wao. Hali si nzuri katika miundombunu ya shule kama vile uhaba wa madarasa, madawati na matundu ya vyoo.

Kwa nini Wabunge wa Mkoa wa Tanga wamepata daraja D?

Vigezo vya upimaji	Viwango vya Kitaifa	Hali halisi katika Mkoa	Alama ilizopata (1-5)
Uandikishaji	95% zaidi	119.6%	5
Ikama ya walimu	1:40	1:46	3
Uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi	1:25	1:49	0
Uwiano wa darasa kwa wanafunzi	1:40	1:75	0
Uhaba wa madawati	0%	33.5%	0
Ufaulu wa wanafunzi	100%	35.8%	2
Wanaojiunga kidato cha kwanza	100%	52.8%	3
Jumla ya alama			**13**
Wastani wa alama			**1.9**
Wastani wa alama kwa asilimia			**38%**
DARAJA			**D**

SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania.
Simu (255 22) 2151852 • Faksi (25522) 2152449
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org